**HALMASHAURI YA JIJI DODOMA**
**MTIHANI WA SAYANSI PACKAGE NAMBA 01 - DARASA LA SABA**

**05**

**SAYANSI**

**MUDA SAA 1.30** **APRILI 2020**

**Maelekezo**


1. Mtihani huu una jumla ya maswali arobaini na tano (45) wenye sehemu A na B. Jibu maswali yote.
2. Jibu sawali la 1 – 40 kwa kutumia karatasi ya kujibia kwa kujaza herufi ya jibu lililosahihi
3. Jibu swali la 41 – 45 kwa kujaza nafasi zilizo wazi.
4. Andika Jina lako kamili na Jina la Shule.

## SEHEMU A: CHAGUA HERUFI YA JIBU SAHIHI

1. Kitendo cha mmea kufyonza maji kutoka kwenye udongo kwa kutumia mizizi huitwa _____
(a) transipiresheni (b) umande (c) osmosis (d) photosinthesis (e) phototropizimu

2. Viumbe wafuatao wapo katika kundi lipi la Wanyama? Nyoka, Kobe na Kinyonga
(a) Reptilia (b) Amfibia (c) Mamalia (d) Ndege (e)wadudu

3. Katika mchoro wa Ua ufuatao, ni sehemu ipi huvutia wadudu kwa ajili ya uchavushaji?




(a) 1 (b) 2 (c) 3 (d) 4 (e) 5


4. Muunganiko wa ogani zinazofanya shughuli moja au zaidi kwa kutegemeana huitwa (a) ogani (b) tissue (c) mfumo (d) nukleasi (e) Seli

5. Ni aina ipi ya chakula mmeng'enyo wake huanzia mdomoni ___
(a) Matunda (b) protini (c) mafuta (d) vitamini (e) kabohaidreti

6. Mazoezi ni njia mojawapo ya kupunguza _____

(a) kutapika (b) kuharisha (c) kuzimia (d) msukumo mkubwa wa damu
(e) Kifua Kikuu

7. Sehemu iliyooneshwa kwa herufi **N** kwenye mchoro ufuatao inaitwa _______




(a) Dendriti (b)Aksoni/axon (c)Saitoplaziamu (d)Nukliasi (e) Neva

8. Sehemu ya ubongo inayotawala matendo yasiyo ya hiari ni __ (a) ubongo wakati (b)ubongo wa nyuma (c)neva (d)ubongo wa mbele (e)uti wa mgongo

9. Ateri zote husafirisha damu safi isipokuwa _____ (a) ateri za renali
(b) ateri za pulmonari (c) ateri za koronari (d) ateri za jugular (e) ateri za mesentari

10. Uchafu uliochujwa na figo hupelekwa kwenye kibofu kupitia mrija uitwao _______
(a) bronchiole (b) urethra (c) eusofagasi (d) ureta (e) falopiani

11. Ni virutubisho gani vinapatikana kwenye mboga za majani? ________
(a) vitamini (b) protini (c) fati (d) wanga (e) madini

12. Ili mmea uweze kutengeneza chakula chake wakati wa mchana unahitaji gesi aina gani? (a) Oksijeni (b) Naitrojeni (c) Haidrojen (d) Kabondaoksaidi
(a) Kabonmonoksaidi

13. Mifupa miwili inayotengeneza sehemu za muundi (ugoko) wa mguu ni _____ na _____
(a) Fibula na Tibia (b) Humas na kraviko (c) Skapla na stenamu (d) Nyundo na fuawe
(e) Fupaja na radiasi

14. Vyakula vya aina gani miongoni mwa hivi hutusaidia kulinda afya zetu?
(a) Samaki na maziwa (b) Maharage na karanga (c) Uji mgumu na ndizi
(c) Mayai na viazi (e) Matunda na mboga

15. Moja kati ya magonjwa yafuatayo hayawezi kukingwa kwa chanjo_____
(a) pumu (b) surua (c) kifua kikuuu (d) pepopunda (e) kifaduro

16. Huduma ya kwanza ifaayo kutolewa kwa mtu aliyekunywa sumu ni _____

(a) Kumfanya aitapike (b) kumnywesha maziwa (c) kumnywesha sukari
(d) kumwahisha hospitali (e) Kumlaza chali


17. Anemia ni ugonjwa unaoweza kuepukwa kwa kuongeza _____ katika mlo
(a) Nyama na Samaki (b) Nafaka na Maharagwe (c) Matunda na mboga za majani
(d) wali na njegele (e) maziwa na mkate


18. Watu walioathirika na virusi vya UKIMWI huhitaji yote yafuatayo isipokuwa_____
(a) Upendo na msaada (b) Mlo kamili (c) Kutibu magonjwa nyemelezi
(d) kuwanyanyapaa (e) usafi


19. Nini kitatokea endapo wanyama walao nyama wataongezeka kwa idadi ukilinganisha na wanyama walao majani kwenye ikolojia? (a) Majani yatapungua
(b) Majani kunyauka (c) Upatikanaji wa majani utalingana (d) Majani yataongezeka
(e) Majani yote yataliwa


20. Mfano wa badiliko la kikemikali ni ..................... (a) maji kuwa mvuke
(b) Tunda kuiva (c)kuyeyuka kwa sukari (d) Barafu kuyeyuka
(e) kutanuka kwa chuma


21. Upi kati ya michoro ifuatayo unaonesha hali halisi ya kuakisiwa kwa mwale wa mwanga?

(a) 

(B) 

( (( 









22. Yurea, maji na chumvichumvi hutolewa kwa wingi wakati wa joto kupitia_____
(a) figo (b) kukojoa (c) mapafu (d) ini (e) ngozi

23. Watu wanaoishi katika maeneo yenye baridi wanashauriwa kula vyakula vyenye mafuta kwa sababu ya _____
(a) hulinda mwili (b) hujenga mwili (c) vinaupa mwili joto (d) vinaupa mwili nguvu (e) vinafanya baadhi ya watu kuwa wanene.

24. Waya wa ethi hukinga nyumba dhidi ya radi. Alama ipi inawakilisha kikinga majanga hicho?_

(a)  (b)  (c)  (d)  (e) 

25. Vitu vipi kati ya vifuatavyo huweza kutenganishwa kwa sumaku?______

(a) Unga wa ayani na mchanga (b) unga na vipande vya karatasi

(c) pini za plasiki na mchanga (d) unga wa kioo na mchanga (e) mchanga na mchele

26. ………………… Ni sehemu ya mbegu inayojitokeza kwanza wakati wa kuchipua

(a) Testa (b) Kianza mche (c) Ganda la ndani (d) Kianza mzizi (e) Maikropail

27. Mahusiano kati ya viumbe hai na visivyo hai katika mazingira hujulikana kama ____ (a) Kutegemeana (b) Mlishano (c) ikolojia (d) mfumo (e) uwiano wa kiasili

28. Umeme wa ampia 0.6 umepita kwenye waya wenye ukinzani wa 6hm.Nini volteji yake? (a) 36V (b) 10V (c) 0.6V (d) 3.6V (e) $^{1}/6$V

29. Zifuatazo ni mashine tata isipokuwa:-

(a) Cherehani (b) mkasi (c) Baiskeli (d) Gari ( e) Kikokoteo

30. Ni nani mwenye jukumu la kutoa huduma ya kwanza?

(a) Madaktari (b) wauguzi (c) wakunga (d) mtu yeyote mwenye ujuzi wa kufanya hivyo (e) watumishi wa chama cha Msalaba mwekundu

31. Katika spektramu ya mwanga, rangi ya mwisho kupinda ni __________

(a) urujuani (b) nyekundu (c) hudhurungi (d) kijani (e) njano

32. Ugonjwa unaosababisha fizi kutokwa damu ni __________

(a) Skavi (b) UKIMWI (c) maleria (d) Goita (e) shinikizo la damu la juu

33. Ni hatua gani ya uchunguzi wa kisayansi hukanusha au kukubali dhanio/bunio la utafiti? (a) Kugundua tatizo (b) kufanya jaribio (c) kukusanya data

(d) kutafsiri data (e) kuandaa taarifa

34. Kutokana na mchoro ufuatao, kundi lipi linawakilishwa na herufi R?_______

**Njia za maambukizi ya virusi vya UKIMWI**

Kunyonyesha | kujamiiana | kuongezewa damu | kuchangia vitu vyenye ncha kali

M | N | R | P

(a) Watoto (b) wagonjwa (c) wasichana (d) wauguzi (e) madaktari

35. Bwana Tobiko aling'atwa na nyoka mwenye sumu kali. Ni sehemu gani ya moyo itafikiwa ya kwanza na sumu? (a) Ventriko ya Kushoto (b) Ventriko ya kulia (b) Auriko ya kushoto (d) Auriko ya kulia (e) Vena kava

36. Nini hutokea mwanga upitapo katika media tofauti
(a)Husafiri kwa kugawa vitu sehemu mbili (b) kusafiri katika mstali mnyoofu (c) hupinda (d) husafiri ndani ya maji kwa kujikunja (e) husafiri na kusababsiha vitu kupinda

37. Homoni zinazoandaa mwili kukabiliana na hatari huitwa ____
(a) adrenali (b) insulini (c) sailoksini (d) tezi (e) projestroni

38. Mmojawapo kati ya mimea ifuatayo ina tabia ya uchavushaji peke
(a) Papai (b) karafuu (c) mahindi (d) korosho (e) mgomba

39. Ipi kati ya sentensi zifuatazo SIO SAHIHI kuhusu UKIMWI
(a) UKIMWI huambukizwa kwa kupeana damu isiyopimwa
(b) UKIMWI unawapata watu wa rika zote
(c) watu wenye kansa wanaweza kuwa wameathirika na UKIMWI
(d) vyakula vyenye protini na Vitamini ni nzuri kutumiwa na mgonjwa wa UKIMWI (e) UKIMWI unaweza kuambukizwa na mtu yeyote.

40.. Sikio la mwanadamu limegawanyika katika sehemu kuu ngapi ?
A mbili B nne C sita D tatu D tano

## SEHEMU B: JAZA NAFASI WAZI

1. Aina ya metali inayopatikana katika hali ya kimiminika ni ………………
2. Chembe ndogo sana za kijani ambazo hupatikana katika saitoplazimu ya seli ya mmea huitwa ……………………………………
3. Kifaa kinachotumika kupima mgandamizo wa hewa huitwa ……………
4. Ili kugomboa chumvi katika majimaji utafanya nini? ……………………………

5. Hii ni aina gani ya transifoma? ………………………………………….

